# SHETANI KUSHINDANA NA KRISTO

- Kuna Ushindi Mkubwa Juu Ya Pepo Wabaya!
- Kamwe Usiabudu Yule Mdanganyifu Shetani, Au Mapepo.
- Wote Wameangamia Milele Wanao Pokea "Alama Ya Mnyama" Kwenye Mkono Wao Au Paji la Uso Ili Waweze Kununua Au Kuuza

Kimebuniwa Na Watson Goodman

Bure—Hakiuzwi

## SHETANI KUSHINDANA NA KRISTO

Shetani, anaelezwa katika Neno la Mungu kama "mfalme wa Ulimwengu Huu," ni adui mkuu wa Mungu na wa kiumbe kikuu cha Mungu—mwanadamu. Sisi wanadamu tuko katika uwanja wa vita pasipo tumaini. Vita viaendelea kati ya Kristo na Shetani. Lazima tuchague kati ya hawa wawili nani atakuwa bwana wetu binafsi milele, Kristo Muumbaji—ambaye ni Emanueli (Mungu pamoja nasi)—au Shetani, kiumbe—ambaye ni mfalme wa maasi yote kinyume cha Mungu. Kupitia kifo chake na ufufuo, Kristo alipata ushindi kamili kwa wote watakao mwamini kikweli.

Shetani hujaribu kwa njia nyingi kudanganya na kuongoza watu vibaya. Ibada ndio lengo lake. Kristo, Muumba wetu, anastahili ibada yote. Tunajitambulisha na yule tunaemuabudu. Juhudi za mwisho za Shetani kuwanasa watu ulimwenguni kote zinalenga: (1)Kuwa huru tokana na Mungu, (2)Utiifu kwa mapepo, (3)Ibada ya "mtu wa dhambi", (4)Ibada ya "sanamu" Yake na, (5)alama katika mwili inayotakikana kwa kununua na kuuza. Jihadhari na haya yote!

—Watson Goodman (1920-2002)



### *Mungu Alimwuumba Lusifa Kuwa Katika Cheo Cha Juu Mbinguni*

Bwana MUNGU asema hivi; Wewe wakitia muhuri kipimo, umejaa hekima, na ukamilifu wa uzuri. Ulikuwa ndani ya Adeni, bustani ya Mungu; kila jiwe la thamani lilikuwa kifuniko chako, . . . kazi ya matari yako na filimbi zako ilikuwa ndani yako; katika siku ya kuumbwa kwako zilitengenezwa tayari.

### *Alikuwa Karibu Na Enzi Ya Mungu*

Wewe ulikuwa kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye; nami nalikuweka hata ukawa juu ya mlima mtakatifu wa Mungu, umetembea huko na huko kati ya mawe ya moto.

### *Aliumbwa Kikamilifu*

Ulikuwa mkamilifu katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa, hata uovu ulipoonekana ndani yako.

### *Mungu Hutupa Dhambi Inje*

Kwa . . . uchuuzi wako watu walikujaza udhalimu ndani yako, nawe umetenda dhambi; kwa sababu hiyo nimekutoa kwa nguvu katika mlima wa Mungu, kama kitu kilicho najisi; nami nimekuangamiza, Ewe kerubi ufunikaye, utoke katika mawe hayo ya moto.

—Ezekieli 28:12b-16



Kiburi hutangulia uangamivu; na roho yenye kutakabari hutangulia maanguko. —Mithali 16:18

Moyo wako uliinuka kwa sababu ya uzuri wako; umeiharibu hekima yako kwa sababu ya mwangaza wako; nimekutupa chini, nimekulaza mbele ya wafalme, wapate kukutazama.

### *Adhabu Ya Muasi*

Kwa wingi wa maovu yako, katika uovu wa uchuuzi wako, umepatia unajisi patakatifu pako; basi nimetokeza moto kutoka ndani yako, nao umekuteketeza, nami nimekufanya kuwa majivu juu ya nchi, machoni pa watu wote wakutazamao. Wote wakujuao kati ya kabila za watu watakustaajabia; umekuwa kitu cha kutisha, wala hutakuwapo tena hata milele. —Ezekieli 28:17-19

### *Kiumbe Chochote Kitakuwa Chini Ya Muumba Wake*

Mtumikieni BWANA kwa furaha; njoni mbele zake kwa kuimba; jueni kwamba BWANA ndiye Mungu; ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake; tu watu wake, na kondoo wa malisho yake.

—Zaburi 100:2, 3

Kumcha BWANA ndio mwanzo wa hekima, wote wafanyao hayo wana akili njema, sifa zake zakaa milele. —Zaburi 111:10



### *Nia Yake Kinyume Cha Nia Ya Mungu*

Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa, ewe uliyewaangusha mataifa! Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, katika pande za mwisho za kaskazini. Nitapaa kupita vimo vya mawingu, nitafanana na yeye Aliye juu.

### *Hufanya Uharibifu Duniani*

Lakini utashushwa mpaka kuzimu; mpaka pande za mwisho za shimo. Wao wakuonao watakukazia macho, watakuangalia sana, wakisema, Je! huyu ndiye aliyeitetemesha dunia, huyu ndiye aliyetikisa falme; aliyeufanya ulimwengu ukiwa, akaipindua miji yake; asiyewafungua wafungwa wake waende kwao?

Wafalme wote wa mataifa wamezikwa wote kwa heshima, kila mmoja ndani ya nyumba yake mwenyewe; bali wewe umetupwa mbali na kaburi lako, kama chipukizi lililochukiza kabisa; kama vazi la wale waliouawa, wale waliochomwa kwa upanga, wale washukao mpaka misingi ya shimo.

—Isaya 14:12-19a

(Tazama Namna Lusifa alisema "Nita" mara tano katika Isa 14:13 na 14 katika ukurasa 3)

Akawaambia, Nilimwona Shetani, akianguka kutoka mbinguni kama umeme. —Luka 10:18

### Katika Malaika Wanao Mfuata Shetani

. . . Mungu hakuwaachilia malaika waliokosa, bali aliwatupa shimoni, akawatia katika vifungo vya giza, walindwe hata ije hukumu. —2 Petro 2:4

### Katika Watu Shetani Anaoweza Kuwadanganya

Wala asiwe mtu aliyeongoka karibu, asije akajivuna akaanguka katika hukumu ya Ibilisi. —1 Timotheo 3:6

### Shetani Hupata Mamlaka Juu Ya Mwanadamu

. . . maana mtu akishindwa na mtu huwa mtumwa wa mtu yule. —2 Petro 2:19b

### Mbinguni Lazima Kuwe Na Nia Moja Tu—Nia Kamilifu Ya Mungu

Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu. —Warumi 12:2



Mimi ni BWANA, Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa. Usiwe na miungu mingine ila mimi. —Kumbukumbu La Torati 5:6, 7

Mpeni BWANA utukufu wa jina lake; leteni sadaka, mje mbele zake; mwabuduni BWANA kwa uzuri wa utakatifu. —1 Mambo Ya Nyakati 16:29

Ndipo Yesu alipomwambia, Nenda zako, Shetani; kwa maana imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake. —Mathayo 4:10

Nami nikaanguka mbele ya miguu yake (Yamalaika), ili nimsujudie; akaniambia, Angalia, usifanye hivi; mimi ni mjoli wako na wa ndugu zako walio na ushuhuda wa Yesu. Msujudie Mungu. —Ufunuo 19:10a

Njoni, tuabudu, tusujudu, tupige magoti mbele za BWANA aliyetuumba. —Zaburi 95:6

*(Tazama Mwa 1:27.)*

### Waliodanganywa Huabudu Mwasi

Dunia yote ikamstaajabia mnyama yule. Wakamsujudu yule joka kwa sababu alimpa huyo mnyama uwezo wake; nao wakamsujudu yule mnyama. Wakisema, Ni nani afananaye na mnyama huyu? Tena ni nani awezaye kufanya vita naye? —Ufu. 13:3b, 4



### Shetani Na Mapepo Wanatamani Ibada

Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mlima mrefu mno, akamwonyesha milki zote za ulimwengu, na fahari yake, akamwambia, Haya yote nitakupa, ukianguka kunisujudia. —Mathayo 4:8, 9

Na wanadamu waliosalia, wasiouawa kwa mapigo hayo, hawakuzitubia zile kazi za mikono yao, hata wasiwasujudie mashetani, na sanamu za dhahabu na za fedha na za shaba na za mawe na za miti, zisizoweza kuona wala kusikia wala kuenenda. —Ufunuo 9:20

### Mungu Huangamiza Waabudu Kama Hao

. . . pakawa na jipu baya, bovu, juu ya wale watu wenye chapa ya huyo mnyama, na wale wenye kuisujudia sanamu yake. Bahari ikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake; na Mauti na Kuzimu zikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake. Wakahukumiwa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake. Mauti na Kuzimu zikatupwa katika lile ziwa la moto. Hii ndiyo mauti ya pili, yaani, hilo ziwa la moto. —Ufunuo 16:2b na 20:13, 14

Mimi ni BWANA; ndilo jina langu; na utukufu wangu sitampa mwingine, wala sitawapa sanamu sifa zangu. —Isaya 42:8



### Malaika Wa Bwana Wanaguvu Zaidi Kuliko Malaika Walioanguka Wa Shetani

Mhimidini BWANA, enyi malaika zake, ninyi mlio hodari, mtendao neno lake, mkiisikiliza sauti ya neno lake. —Zaburi 103:20

Kulikuwa na vita mbinguni; Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka, yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake; na hawakushinda, wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni. —Ufunuo 12:7, 8

### Malaika Watakatifu Wa Mungu Huwahudumia Na Kuwalinda Watu Wa Bwana

Je! hao wote si roho watumikao, wakitumwa kuwahudumu wale watakaourithi wokovu? —Waebrania 1:14

Kwa kuwa atakuagizia malaika zake wakulinde katika njia zako zote. —Zaburi 91:11

### Malaika Walioanguka (mapepo, mashetani) wamekusudia Kupeleka Mtu Jehanamu

. . . akachukua pepo wengine saba, walio waovu kuliko yewe mwenyewe . . . . —Luka 11:26b

Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani. —1 Timotheo 4:1



### Binadamu, Ameumbwa Katika Mfano Wa Mungu

Alipokuwa katika kumwendea, pepo akambwaga chini, akamtia kifafa. Yesu akamkemea pepo mchafu, akamponya mtoto, akamrudishia babaye. —Luka 9:42

### Kristo (Mungu katika Mwili), pamoja Na Wokovu Katika Utu Wake Binafsi Na Damu Ya Uungu

Ndipo Herode, . . . alighadhabika sana, akatuma watu akawaua watoto wote wanaume waliokuwako huko Bethlehemu . . .tangu wenye miaka miwili na waliopungua, kwa muda ule aliouhakikisha kwa wale mamajusi. —Mathayo 2:16

### Neno La Mungu—Shetani Hulipotosha

Ati! hivi ndivyo alivyosema Mungu . . . ? Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa. —Mwanzo 3:1b, 4

### Taifa Teule La Mungu, Israeli

Na joka yule alipoona ya kuwa ametupwa katika nchi, alimwudhi mwanamke yule aliyemzaa mtoto mwanamume. —Ufunuo 12:13

### Wazaliwa-Kiroho Waaminio

. . . mshitaki wenu Ibilisi, . . . huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze. —1 Petro 5:8



### Huigiza Alama Ya Umiliki

Wala hapatakuwa na laana yo yote tena. Na kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo kitakuwamo ndani yake. Na watumwa wake watamtumikia; nao watamwona uso wake, na jina lake litakuwa katika vipaji vya nyuso zao. —Ufunuo 22:3, 4

*(Tazama muigizo wa Shetani, ukurasa 35.)*

### Hugeuza Vibaya Injili Kwa Uongo

. . . lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeuza injili ya Kristo. —Wagalatia 1:7a

### Huigiza Wahuduma Wa Mungu

Maana watu kama hao ni mitume wa uongo, watendao kazi kwa hila, wanaojigeuza wawe mfano wa mitume wa Kristo. Wala si ajabu. Maana Shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru. —2 Wakorintho 11:13, 14

### Miujiza Ya Mungu Kushindana Na Maajabu Ya Uongo

2 The. 2:9; Ufu. 13:13, 14; 19:20

### Shetani Huchukua Mamlaka Watu Wanapo Muabudu Au Kuabudu miungu zake

Ee BWANA, Mungu wetu, mabwana wengine zaidi ya wewe wametumiliki . . . . —Isaya 26:13a

## JITENGE NA SANAMU

Watoto wadogo, jilindeni nafsi zenu na sanamu. —1 Yohana 5:21

Usiwe na miungu mingine ila mimi. Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu. —Kutoka 20:3-5a

### *Miungu Wengine Chukizo Kwa Mungu. Dhabihu Ya Binadamu Marufuku*

Vunjeni kabisa mahali pote walipokuwa wakiitumikia miungu yao mataifa mtakayoyamiliki, juu ya milima mirefu, na juu ya vilima, na chini ya kila mti wenye majani mabichi. Ujiangalie, usije ukanaswa ukawafuata, wakiisha kuangamizwa mbele vako;... Usimtende kama haya BWANA, Mungu wako; kwani kila yaliyo machukizo kwa BWANA, ayachukiayo yeye, wameifanyia miungu yao; kwa maana hata wana wao na binti zao, huiteketezea hiyo miungu yao ndani ya moto. -Kumbukumbu La Torati 12:2, 30a, 31

Je! nimtoe... mzao wa mwili wangu kwa dhambi ya roho yangu? —Mika 6:7b

### *Damu Ya Yesu Huosha Dhambi*

## IBADA YA SANAMU



### *Upumbavu Wa Ibada Ya Sanamu*

Kwa maana waliibadili kweli ya Mungu kuwa uongo, wakakisujudia kiumbe na kukiabudu badala ya Muumba anayehimidiwa milele. Amina. —Warumi 1:25

Lakini Mungu wetu yuko mbinguni, alitakalo lote amelitenda. Sanamu zao ni fedha na dhahabu, kazi ya mikono ya wanadamu. Zina vinywa lakini hazisemi, zina macho lakini hazioni, zina masikio lakini hazisikii, zina pua lakini hazisikii harufu, mikono lakini hazishiki, miguu lakini haziendi, wala hazitoi sauti kwa koo zake. Wazifanyao watafanana nazo, kila mmoja anayezitumainia. —Zaburi 115:3-8

### *Ibada Ya Sanamu Ni Ibada Ya Shetani*

... ikimbieni ibada ya sanamu. Sivyo, lakini vitu vile wavitoavyo sadaka wavitoa kwa mashetani, wala si kwa Mungu; nami sipendi ninyi kushirikiana na mashetani. Hamwezi kunywea kikombe cha Bwana na kikombe cha mashetani. —1 Wakorintho 10:14b na 20

### *Adhabu Ya Ibada Ya Sanamu*

Waabuduo sanamu, ... sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili. —Ufunuo 21:8b



## IBADA YA SANAMU (SHETANI) IMECHUKIWA NA MUNGU

### *Mungu Aliangamiza Mataifa Kwa Sanamu Zao—Usiweke Sanamu Ndani Ya Nyumba Yako!*

Na wafalme wao atakutilia mkononi mwako, nawe utalipoteza jina lao litoke chini ya mbingu; hapana mtu atakayeweza kusimama mbele yako, hata utakapokwisha kuwaangamiza. Sanamu za kuchonga za miungu yao mtaziteketeza kwa moto;... maana ni machukizo kwa BWANA, Mungu wako; na machukizo usitie ndani ya nyumba yako, usije wewe kuwa kitu cha haramu mfano wake. —Kumbukumbu La Torati 7:24-26a

### *Ni Kwa Nini Wengi Katika Taifa Teule La Mungu Walipagawa Pepo Wakati Wa Huduma Ya Kristo?*

Wakazitumikia sanamu zao, nazo zikawa mtego kwao. Naam, walitoa wana wao na binti zao kuwa dhabihu kwa mashetani. Hasira ya BWANA ikawaka juu ya watu wake, akauchukia urithi wake. —Zaburi 106:36, 37, na 40

Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao. —Kutoka 20:5

## UCHAWI WOWOTE NI DHAMBI



Usimwache mwanamke mchawi kuishi. —Kutoka 22:18

Nami nitakatilia mbali uchawi, usiwe mkononi mwako; wala hutakuwa tena na watu wenye kutabana. —Mika 5:12

Kwani kuasi ni kama dhambi ya uchawi, na ukaidi ni kama ukafiri na vinyago; kwa kuwa umelikataa neno la BWANA, yeye naye amekukataa wewe usiwe mfalme. —1 Samweli 15:23

Utakapokwisha kuingia katika nchi akupayo BWANA, Mungu wako, usijifunze kutenda kwa mfano wa machukizo ya mataifa yale. Asionekane kwako mtu ampitishaye mwanawe au binti yake kati ya moto, wala asionekane mtu atazamaye bao, wala mtu atazamaye nyakati mbaya, wala mwenye kubashiri, wala msihiri, wala mtu alogaye kwa kupiga mafundo, wala mtu apandishaye pepo, wala mchawi, wala mtu awaombaye wafu. Kwa maana mtu atendaye hayo ni chukizo kwa BWANA; kisha ni kwa sababu ya hayo BWANA, Mungu wako, anawafukuza mbele yako. —Kumbukumbu La Torati 18:9-12

**Uramali:** Ujuzi wa Kutabiri Mambo ya siku za usoni kwa kutumia mazingaombwe kuwaleta roho za waliokufa; Uchawi.



## KUELEZA MAMBO YA SIKU ZA USONI KWA MSAADA WA MASHETANI

### *Mungu Amekataza Unajimu, Uchawi, Kuchanja na Alama Kwenye Mwili*

Msile kitu cho chote pamoja na damu yake; wala msifanye kuloga, wala kutumia utambuzi. Msichanje chale yo yote katika nyama ya miili yenu kwa ajili ya wafu, wala msiandike alama miilini mwenu; mimi ndimi BWANA. —Mambo Ya Walawi 19:26 na 28

Basi, ... msisikilize manabii wenu, wala wabashiri wenu, wala ndoto zenu, wala watambuzi wenu, wala waganga wenu. —Yeremia 27:9a

Nami nitakuwa shahidi mwepesi juu ya wachawi, na ... wazinzi, na ... waapao kwa uongo .... —Malaki 3:5b

Kwa maana vinyago vimenena maneno ya ubatili, nao waaguzi wameona uongo; nao wameleta habari za ndoto za uongo, wafariji bure. —Zekaria 10:2a

### *Mwamini Mchungaji Wa Kweli*

Yesu Akasema, "Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi." —Yohana 14:1

**Uaguzi:** Kueleza Mambo ya siku za usoni au yasiojulikana kwa njia za udanganyifu. **Uchawi:** Uganga unaofanywa kwa msaada wa pepo wachafu.

## KATAA NAMNA ZOTE ZA UAGUZI



### *Kuagua Na roho za uaguzi*

Na wakati watakapokuambia, Tafuta habari kwa watu wenye pepo na kwa wachawi; waliao kama ndege na kunong'ona; je! haiwapasi watu kutafuta habari kwa Mungu wao? —Isaya 8:19a

### *Kwa kutumia viungo vya mwili, sanamu*

Maana mfalme wa Babeli alisimama penye njia panda, penye kichwa cha njia hizo mbili, ili atumie uganga; aliitikisa mishale huko na huko, akaziuliza terafi, akayatazama maini. —Ezekieli 21:21

### *Kuagua Kwa Vijiti*

Watu wangu hutaka shauri kwa gongo lao, na fimbo yao huwahubiri mambo; maana roho ya uzinzi imewakosesha, nao wamekwenda kuzini mbali na Mungu wao. —Hosea 4:12

### *Adhabu Ya Uaguzi*

Basi Sauli alikufa kwa sababu ya kosa lake alilomkosa BWANA, kwa sababu ya neno la BWANA, asilolishika; na tena kwa kutaka shauri kwa mwenye pepo wa utambuzi, aulize kwake, asiulize kwa BWANA. —1 Mambo Ya Nyakati 10:13, 14a

Na hao waonaji watatahayarika, na wenye kubashiri watafadhaika; ... kwa maana hapana jawabu la Mungu. —Mika 3:7

## NAMNA AMBAZO MFALME WA ULIMWENGU HUU HUFANYA KAZI

### *Wapagani Hufuata Unajimu*

**BWANA asema hivi, Msijifunze njia ya mataifa, wala msishangae kwa sababu ya ishara za mbinguni; maana mataifa hushangaa kwa sababu ya ishara hizo.**
—Yeremia 10:2

Usitumainie Barua au vitu vya kujipatia "Bahati" wala usijitoe kwa miziki ya kishetani au picha mbaya. **"Sitaweka mbele ya macho yangu Neno la uovu."** —Zaburi 101:3a. Achana na kiburi, unafiki, na dini iliokufa.

**Ole wenu . . . kwa kuwa mmefanana na makaburi yaliopakwa chokaa, . . . kwa nje yaonekana kuwa mazuri, bali ndani yamejaa . . . uchafu wote. Vivyo hivyo ninyi nanyi, kwa nje mwaonekana na watu kuwa wenye haki, bali ndani mmejaa unafiki na maasi.** —Mathayo 23:27, 28

### *Kujiuwa Kunatoka Kwa Shetani*

Usiamini uongo wa Shetani au mapepo kwamba kujiuwa kunaleta uhuru kutokana na shida na uovu! **"Usiue."** —Kutoka 20:13.

### *Kristo Pekee Huweka Huru Kutokana Na Uovu*

**BWANA ni nguvu zangu, na wimbo wangu; naye amekuwa wokovu wangu.** —Kutoka 15:2a

## JIHADHARI NA UJUMBE WA SHETANI



### *Kupitia Manabii Wa Uongo*

**Ndipo BWANA akaniambia, Hao manabii wanatabiri uongo kwa jina langu mimi; mimi sikuwatuma, wala sikuwaamuru, wala sikusema nao; wanawapeni unabii wa maono ya uongo, na uaguzi, na neno la ubatili, na hadaa ya mioyo yao.** —Yeremia 14:14

**Kwa maana wataondoka Makristo wa uongo, na manabii wa uongo, watatoa ishara na maajabu, wapate kuwadanganya, kama yamkini, hata hao wateule.**
—Marko 13:22

### *Kupitia Kuzungumza Na Wafu*

Kwa uvuvio wa Mungu, Mfalme Daudi Alisema Juu Ya Mwanawe, **"Lakini sasa amekufa, . . . yeye hatanirudia mimi."** —2 Samweli 12:23

Usizungumze na pepo wabaya, isipokuwa kwa kuwaamuru Kwa Jina la Kristo waondoke. Usiweke tumaini katika kusoma viganja, bao, hirizi, uganga.

### *Haribu Sanamu, Vitabu Vya Shetani*

**Na watu wengi katika wale waliotumia mambo ya uganga wakakusanya vitabu vyao, wakavichoma moto mbele ya watu wote; wakafanya hesabu ya thamani yake, wakaona ya kwamba yapata fedha hamsini elfu.** —Matendo 19:19
*(Soma Mwa. 35:2-5.)*



## KRISTO ALIUMBA UHUSIANO WA MUME-MKE SHETANI HUPOTOSHA UHUSIANO HUU

### *Uhusiano Wa Mume-Mke Umeruhusiwa Katika Ndoa Pekee*

**Na ule ubavu alioutwaa katika Adamu BWANA Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu. Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja.**
—Mwanzo 2:22 na 24

**Lakini wale waliokwisha kuoana nawaagiza; wala hapo si mimi, ila Bwana; mke asiachane na mumewe; lakini, ikiwa ameachana naye, na akae asiolewe, au apatane na mumewe; tena mume asimwache mkewe.**
—1 Wakorintho 7:10, 11

**Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi; kwa maana waasherati na wazinzi Mungu atawahukumia adhabu.**
—Waebrania 13:4

### *Shetani Anahusika Na Kutotii*

**Atendaye dhambi ni wa Ibilisi; kwa kuwa Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo.** —1 Yohana 3:8a

### *Wewe Ni Wa Yule Unae Mtii*

**Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii.** --Warumi 6:16a

## UASHERATI NA UZINZI NI KUMUASI MUNGU



**Usizini.** —Kutoka 20:14

**Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu, mwepukane na uasherati.**
—1 Wathesalonike 4:3

**Na mtu aziniye na mke wa mtu mwingine, naam, yeye aziniye na mke wa jirani yake, mtu mume aziniye, na mwanamke aziniye, hakika watauawa.**
—Mambo Ya Walawi 20:10

### *Dhambi Juu Ya Mwili Wako*

**Mwili si kwa zinaa, bali ni kwa Bwana, naye Bwana ni kwa mwili. Je! hamjui ya kuwa miili yenu ni viungo vya Kristo? Basi nivitwae viungo vya Kristo na kuvifanya viungo vya kahaba? Hasha! Ikimbieni zinaa. Kila dhambi aitendayo mwanadamu ni nje ya mwili wake; ila yeye afanyaye zinaa hutenda dhambi juu ya mwili wake mwenyewe.**
—1 Wakorintho 6:13b, 15 na 18

### *Wazazi Wajikinge Na Dhambi Ya Uasherati*

**Usimnajisi binti yako, ili kumfanya awe kahaba; isiwe hiyo nchi kuuandama ukahaba, na nchi kujawa na uovu mkuu.**
—Mambo Ya Walawi 19:29

**Uasherati:** Uhusiano wa kimwili kati ya mume-mke kabla ya ndoa.
**Uzinzi:** Uhusiano wa kimwili na mtu mwingine mbali na yule umefunga nae.



## SHETANI ALISHINDWA KWA KIFO CHA KRISTO

**Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa.**
—1 Wakorintho 15:22

**Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi, awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa.**
—Waebrania 2:14, 15

**Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi.** —1 Yohana 3:8b

**Akiisha kuzivua enzi na mamlaka, na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba huo.** —Wakolosai 2:15

### *Kudumu Kwetu Milele Katika Kristo*

**Ambaye alituokoa akatuita kwa mwito mtakatifu, si kwa kadiri ya matendo yetu sisi, bali kwa kadiri ya makusudi yake yeye na neema yake. Neema hiyo tulipewa katika Kristo Yesu tangu milele, na sasa inadhihirishwa kwa kufunuliwa kwake Mwokozi wetu Kristo Yesu; aliyebatili mauti, na kuufunua uzima na kutokuharibika, kwa ile Injili.**
—2 Timotheo 1:9, 10

## USHINDI WA MKRISTO JUU YA SHETANI



**Mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze. . . . mpingeni huyo, mkiwa thabiti katika imani.**
—1 Petro 5:8b, 9a

**Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani. Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. . . . mpate kuweza kushindana siku ya uovu, . . . hali mmejifunga kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani, na kufungiwa miguu . . . Injili ya amani; zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu; . . . mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha.**
—Waefeso 6:11-18a

**Basi mtiini Mungu. Mpingeni Shetani, naye atawakimbia.**
—Yakobo 4:7

**Aliye ndani yenu (Kristo) ni mkuu kuliko yeye (Shetani) aliye katika dunia.** —1 Yohana 4:4b

Sababu Shetani Hutoroka: Kristo Yuko Ndani Yako!

### *Yeye Ni Sauti Ya Mungu*

Mungu, . . . mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu. —Waebrania 1:1a, 2

Wakashangaa mno kwa mafundisho yake; kwa maana alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye amri, wala si kama waandishi. —Marko 1:22

Naye akampa amri ya kufanya hukumu kwa sababu ni Mwana wa Adamu. —Yohana 5:27

Lakini kwetu sisi Mungu ni mmoja tu, aliye Baba, ambaye vitu vyote vimetoka kwake, nasi tunaishi kwake; yuko na Bwana mmoja Yesu Kristo, ambaye kwake vitu vyote vimekuwapo, na sisi kwa yeye huyo. —1 Wakorintho 8:6

Naye yupo mkono wa kuume wa Mungu, amekwenda zake mbinguni, malaika na enzi na nguvu zikiisha kutiishwa chini yake. —1 Petro 3:22

Maana Kristo alikufa akawa hai tena kwa sababu hii, awamiliki waliokufa na walio hai pia. —Warumi 14:9

Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. —Mathayo 28:18



Akaamka, akaukemea upepo, akaiambia bahari, Nyamaza, utulie. Upepo ukakoma, kukawa shwari kuu. —Marko 4:39

### *Aliponya Kwa Mamlaka*

Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi, (hapo amwambia yule mwenye kupooza), Nakuambia, Ondoka, ujitwike godoro lako uende nyumbani kwako. Mara akaondoka, akajitwika godoro lake, akatoka mbele yao wote; hata wakastaajabu wote, wakamtukuza Mungu. —Marko 2:10-12a

Naye mkwewe Simoni, mamaye mkewe, alikuwa kitandani, hawezi homa; na mara wakamwambia habari zake. Akamkaribia, akamwinua kwa kumshika mkono, homa ikamwacha, akawatumikia. —Marko 1:30, 31

### *Kristo Hufukuza Mashetani*

Yule pepo mchafu akamtia kifafa, akalia kwa sauti kuu, akamtoka. Wakashangaa wote, hata wakaulizana, wakisema, Nini hii? Ni elimu mpya! Maana kwa uweza awaamuru hata pepo wachafu, nao wamtii! —Marko 1:26, 27

### *Alifufua Wafu Kwa Uwezo*

Akasema, Kijana, nakuambia, Inuka. Yule maiti akainuka, akaketi, akaanza kusema. Akampa mama yake. —Luka 7:14b, 15



## KRISTO HUWAPA WAFUASI WAKE MAMLAKA NA NGUVU JUU YA NGUVU ZOTE ZA ADUI

Bwana, hata pepo . . . . Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru. Lakini, msifurahi kwa vile pepo wanavyowatii; bali furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa mbinguni. —Luka 10:17b, 19, 20

Akawaita wale Thenashara, akawapa uwezo na mamlaka juu ya pepo wote na kuponya maradhi. —Luka 9:1

Amin, nawaambia, Ye yote atakayeuambia mlima huu, Ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake. —Marko 11:23

Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu. —Wafilipi 4:13

Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya. —Yohana 14:12a

Yesu akamwambia, Ukiweza! Yote yawezekana kwake aaminiye. —Marko 9:23

Na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake. —Waefeso 1:19



### *Wakemee. Waamuru Watoke Katika Jina La Yesu*

Kwa sababu amemwambia, Ewe pepo mchafu, mtoke mtu huyu. Akamwuliza, Jina lako nani? Akamjibu, Jina langu ni Legioni, kwa kuwa tu wengi. Akawapa ruhusa. Wale pepo wachafu wakatoka, wakaingia katika wale nguruwe; nalo kundi lote likatelemka kwa kasi gengeni, wakaingia baharini, wapata elfu mbili; wakafa baharini. —Marko 5:8, 9 na 13

Yesu, . . . akamkemea yule pepo mchafu, akamwambia, Ewe pepo bubu na kiziwi, mimi nakuamuru, mtoke huyu, wala usimwingie tena. Akalia, akamtia kifafa sana, akamtoka; naye akawa kama amekufa; hata wengi wakasema, Amekufa. Lakini Yesu akamshika mkono akamwinua; naye akasimama. Namna hii yaweza kutoka . . . kwa kuomba na kufunga. —Marko 9:25b-27 na 29b

Paulo, . . . akageuka akamwambia yule pepo, Nakuamuru kwa jina la Yesu Kristo, mtoke huyu. Akamtoka saa ile ile. —Matendo 16:18b

Yesu akamkemea, akisema, Fumba kinywa, mtoke. Ndipo yule pepo akamwangusha katikati, akamtoka asimdhuru neno. —Luka 4:35



## JINA KUU LA YESU KRISTO KUPITA MAJINA YOTE

Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi. —Wafilipi 2:9, 10

Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. —Yohana 14:13

Baada ya kuchukua mke wangu na jamii kwa imani kurudi Afrika kwa kazi ya Kristo, niliamka usiku mmoja na pepo mbaya wa kutisha juu yangu. Niliposukuma goti langu kwa goti lake ilinione kama ni kweli, alisukuma goti langu gafla kwa nguvu nyingi, na akanijia kwa haraka zaidi kuelekea shingo yangu aninyonge. Nilikuwa na wakati wa kutamka maneno matatu tu, "Yesu, nisaidie!" Mara moja, akatoweka, na katika miaka 35 tangu hapo, sijawahi kurudiwa na jambo hilo, kunako nguvu za kushangaza katika Jina la Yesu Kristo juu ya Shetani na mapepo wote! Liitie Jina la Kristo kwa wokovu na ukombozi. (Rum. 10:13)

Mwanamke mmoja alimwambia mke wangu pamoja nami kwamba wakati alipokuwa chuoni, kijana mmoja alimchukua kwa matembezi njia ya reli. Katika mahali fulani, alijaribu kumuua, akitaka ionekane kuwa ameuawa na gari la moshi. Dada huyu alipomwamuru katika Jina la Yesu, akawa hana nguvu juu yake. Kwa nguvu za Kristo, alimlazimisha atembee mbele yake kurudi huko chuoni.

Mwanamke mwingine akamwambia mke wangu pamoja nami kwamba, katika siku zake za ujana, pasipo busara, aliwakaribisha nyumbani kwake kundi la Waaguzi. Baada ya hayo, pepo wachafu walianza kusongeza vifaa vya nyumbani huku na huku nyumbani mwake. Katika hali ya kukosa tumaini, aliwafukuza toka nyumbani mwake katika Jina la Yesu. Baadaye, alijitoa kabisa kwa Yesu Kristo.

Usihurumie au kusikitikia Shetani au mapepo. Kusudi lao ni kukupata wewe uwe upande wao badala ya kuwa upande wa Mungu. Mzee Mkristo, akiwa amepatwa na unyonge wa mwili na wasi wasi akilini, alinieleza mambo Shetani alikuwa akimwambia. Alikuwa akifikiria "kumjaribu shetani kama anaweza." Nilimuonyesha kwamba, Shetani ni Hodari kwa kudanganya watu na huwezi kuamini neno analo sema. Nilimkemea Shetani katika Jina Kuu la Yesu Kristo. Mtu huyu akasema, "Ninashukuru umekuja usiku huu." Alionekana mwenye amani katika Kristo majuma matatu yaliofuata kabla ya kufa.

—Watson Goodman

***Kristo Ni Mungu Muumbaji***

Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni viti vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake.
—Wakolosai 1:16

***Kristo Hutoa Nuru Na Amani***

Kuwaangaza wakaao katika giza na uvuli wa mauti, na kuiongoza miguu yetu kwenye njia ya amani. —Luka 1:79

Sasa, Bwana wa amani mwenyewe na awape amani daima.
—2 Wathesalonike 3:16a

***Mapepo Na Shetani Huharibu***

Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu. —Yohana 10:10a

Ole wa nchi . . . ! kwa maana yule Ibilisi ameshuka kwenu mwenye ghadhabu nyingi, akijua ya kuwa ana wakati mchache tu.
—Ufunuo 12:12b

***Shetani Hutoa Giza, Mateso***

Njia ya waovu ni kama giza; hawajui ni kitu gani kiwakwazacho.
—Mithali 4:19

Yule tajiri naye akafa, akazikwa. Basi, kule kuzimu aliyainua macho yake, alipokuwa katika mateso. —Luka 16:22b, 23a



***Kristo Ni Kweli***

Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli. Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli; tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru.
—Yohana 1:14 na 8:31b, 32

***Kristo Ni Mwingi Wa Upendo***

Katika hili tumelifahamu pendo, kwa kuwa yeye aliutoa uhai wake kwa ajili yetu; imetupasa na sisi kuutoa uhai wetu kwa ajili ya hao ndugu. —1 Yohana 3:16

***Shetani Ni Baba Wa Uongo***

Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi, na tamaa za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo; wala hakusimama katika kweli, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo, husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni mwongo, na baba wa huo.
—Yohana 8:44

***Shetani Huchochea Chuki***

Iwapo ulimwengu ukiwachukia, mwajua ya kuwa umenichukia mimi kabla ya kuwachukia ninyi.
—Yohana 15:18

Basi matendo ya mwili ni dhahiri, . . . uadui, . . . hasira.
—Wagalatia 5:19a, 20b



***Kristo Husafisha Nafsi***

Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote. —1 Yohana 1:7

***Kristo Hufungua Kutoka Dhambi***

Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye.
—Warumi 5:9

***Kristo Hutoa Uzima Wa Milele***

Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma. —Yohana 17:3

***Shetani Huchafua Nafsi***

Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna. Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu.
—Wagalatia 6:7, 8a

***Shetani Hushawishi Watu Kutenda Dhambi***

Atendaye dhambi ni wa Ibilisi; kwa kuwa Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo. —1 Yohana 3:8

***Shetani Hukuelekeza Kifo Cha Milele***

Na yale magugu ni wana wa yule mwovu; yule adui aliyeyapanda ni Ibilisi; . . . magugu . . . kuchomwa motoni. —Mathayo 13:38b-40a



***Yeye Ndiye Mfalme Wa Ulimwengu Huu Sasa***

Mimi (Yesu) sitasema nanyi maneno mengi tena, kwa maana yuaja mkuu wa ulimwengu huu, wala hana kitu kwangu. —Yohana 14:30

***Iwapo Mambo Hayaendi Sawa, Mlaumu Yeye***

Hekima hiyo siyo ile ishukayo kutoka juu, bali ni ya dunia, ya tabia ya kibinadamu, na Shetani. Maana hapo palipo wivu na ugomvi, ndipo palipo machafuko, na kila tendo baya. —Yakobo 3:15, 16

***Shetani Anapopata Nafasi, Huharibu Uhuru Wa Kuabudu Kristo Wazi wazi. Yeye Hawezi Kuharibu upendo Wako Wa Moyoni Kwa Kristo. Linda Imani!***

Wakampiga kwa mawe Stefano, naye akiomba, akisema, Bwana Yesu, pokea roho yangu. Akapiga magoti, akalia kwa sauti kuu, Bwana, usiwahesabie dhambi hii. Akiisha kusema haya akalala. Na Sauli alikuwa akiona vema kwa kuuawa kwake. —Matendo 7:59, 60

***Serikali Ya Kristo Ulimwenguni***

Maongeo ya enzi yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe, katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake; kuuthibitisha na kuutegemeza kwa hukumu na kwa haki, tangu sasa na hata milele. —Isaya 9:7a



Basi, ndugu, tunakusihini, kwa habari ya kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo, na kukusanyika kwetu mbele zake. Mtu awaye yote asiwadanganye kwa njia yo yote; maana haiji, usipokuja kwanza ule ukengeufu; akafunuliwa yule mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu; yule mpingamizi, ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu. Hapo ndipo atakapofunuliwa yule asi, ambaye Bwana Yesu atamwua kwa pumzi ya kinywa chake, na kumwangamiza kwa ufunuo wa kuwapo kwake; yule ambaye kuja kwake ni kwa mfano wa kutenda kwake Shetani, kwa uwezo wote, na ishara na ajabu za uongo.
—2 Wathesalonike 2:1, 3, 4, 8-9

Yule joka (Shetani) akampa nguvu zake na kiti chake cha enzi na uwezo mwingi. Akapewa uwezo juu ya kila kabila na jamaa na lugha na taifa.—Ufunuo 13:2b na 7b

Nao wakamsujudu yule mnyama, wakisema, Ni nani afananaye na mnyama huyu? Tena ni nani awezaye kufanya vita naye?
—Ufunuo 13:4b



Naye atanena maneno kinyume chake Aliye juu, naye atawadhoofisha watakatifu wake Aliye juu; naye ataazimu kubadili majira na sheria; nao watatiwa mikononi mwake kwa wakati, na nyakati mbili, na nusu wakati. Lakini hukumu itawekwa, nao watamwondolea mamlaka yake, kuyapoteza na kuyaangamiza, hata milele.
—Danieli 7:25, 26

Akapewa uwezo wa kufanya kazi yake miezi arobaini na miwili. Akafunua kinywa chake amtukane Mungu, na kulitukana jina lake, na maskani yake, nao wakaao mbinguni. Tena akapewa kufanya vita na watakatifu na kuwashinda, akapewa uwezo juu ya kila kabila na jamaa na lugha na taifa. Na watu wote wakaao juu ya nchi watamsujudu, kila ambaye jina lake halikuandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia. Mtu akiwa na sikio na asikie. —Ufunuo 13:5b-9

Piga vita vile vizuri vya imani; shika uzima ule wa milele ulioitiwa, ukaungama maungamo mazuri mbele ya mashahidi wengi.
—1 Timotheo 6:12

## KAMWE USIABUDU SANAMU YA MPINGA KRISTO

*Kiongozi Wa Dini Wa Ulimwengu Asaidia Mpinga Kristo Kuudanganya Ulimwengu.*

Naye awakosesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya mbele ya huyo mnyama, akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama, aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi. Akapewa kutia pumzi katika ile sanamu ya mnyama, hata ile sanamu ya mnyama inene, na kuwafanya hao wote wasioisujudu sanamu ya mnyama wauawe. Yule mnyama akakamatwa, na yule nabii wa uongo pamoja naye, yeye aliyezifanya hizo ishara mbele yake, ambazo kwa hizo aliwadanganya watu wale walioipokea ile chapa ya huyo mnyama, nao walioisujudia sanamu yake; hao wawili wakatupwa wangali hai katika lile ziwa la moto. —Ufunuo 13:14, 15 na 19:20

*Watu Wa Mungu Wakataa Miungu Wengine*

Kama ni hivyo, Mungu wetu tunayemtumikia aweza kutuokoa na tanuru ile iwakayo moto. Bali kama si hivyo, ujue, Ee mfalme, ya kuwa sisi hatukubali kuitumikia miungu yako, wala kuisujudia hiyo sanamu ya dhahabu uliyoisimamisha. —Danieli 3:17a, 18

## MPINGA KRISTO: JITOE AU SHINDA NJAA


Naye awafanya wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao; tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani, jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake. . . . Yeye aliye na akili, . . . maana ni hesabu ya kibinadamu. Na hesabu yake ni mia sita, sitini na sita. —Ufunuo 13:16-18

*Siku Njema Yaja Kwa Waongovu*

Hao ndio wanatoka katika dhiki ile iliyo kuu, nao wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo. Kwa hiyo wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku katika hekalu lake, na yeye aketiye katika kiti cha enzi atatanda hema yake juu yao. Hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga, wala hari iliyo yote. Kwa maana huyo Mwana-Kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga, naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai. —Ufunuo 7:14b-17a

*Heri Kuingia Mbinguni Ukiwa Njaa Kuliko Kuingia Jehanamu Na Tumbo Limeshiba!*


## WATU WOTE WAMEKWISHA ANGAMIA WANAO MUABUDU MPINGA KRISTO, AU KUPOKEA ALAMA YAKE KWENYE MIILI YAO ILI WANUNUE AU KUUZA

Na mwingine, malaika wa tatu, akawafuata, akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake,

Yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo.

Na moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku, hao wamsujuduo huyo mnyama na sanamu yake, na kila aipokeaye chapa ya jina lake.

Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu.

Nikasikia sauti kutoka mbinguni ikisema, Andika, Heri wafu wafao katika Bwana tangu sasa. Naam, asema Roho, wapate kupumzika baada ya taabu zao; kwa kuwa matendo yao yafuatana nao. —Ufunuo 14:9-13

## USHINDI JUU YA ALAMA YA SHETANI NA SANAMU KABLA YA GADHABU YA MUNGU KUJA DUNIANI


Malaika saba wenye mapigo saba ya mwisho; maana katika hayo ghadhabu ya Mungu imetimia. Tena nikaona kitu kama mfano wa bahari ya kioo iliyochangamana na moto, na wale wenye kushinda, watokao kwa yule mnyama, na sanamu yake, na kwa hesabu ya jina lake, walikuwa wamesimama kandokando ya hiyo bahari ya kioo, wenye vinubi vya Mungu. Nao wauimba wimbo wa Musa, mtumwa wa Mungu, na wimbo wa Mwana-Kondoo, wakisema, Ni makuu, na ya ajabu, matendo yako, Ee Bwana Mungu Mwenyezi; Ni za haki, na za kweli, njia zako, Ee Mfalme wa mataifa. Nikasikia sauti kuu kutoka hekaluni, ikiwaambia wale malaika saba, Enendeni, mkavimimine vile vitasa saba vya ghadhabu ya Mungu juu ya nchi. —Ufunuo 15:1b-3 na 16:1

(Ufunuo 16-18: Tauni Saba Na Matokeo.)

Nami nikaona roho zao waliokatwa vichwa kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu, na kwa ajili ya neno la Mungu, . . . nao wakawa hai, wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu. —Ufunuo 20:4b


## MEGIDO, VITA KRISTO AKOMESHA

*Mashetani Wakusanya Mataifa Kupigana*

Hizo ndizo roho za mashetani, zifanyazo ishara, zitokazo na kuwaendea wafalme wa ulimwengu wote, kuwakusanya kwa vita ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi. Wakawakusanya hata mahali paitwapo kwa Kiebrania, Har-Magedoni. —Ufunuo 16:14 na 16

*Kristo Akomboa Ardhi Yake Na Watu Wake Wateule, Israeli*

Angalia, mimi nitafanya Yerusalemu kuwa kikombe cha kuyumba-yumba. Tena itakuwa siku hiyo, nitafanya Yerusalemu kuwa jiwe la kuwalemea watu wa kabila zote; wote watakaojitwika jiwe hilo watapata jeraha nyingi; na mataifa yote ya dunia watakusanyika pamoja juu yake. Hapo ndipo atakapotokea BWANA, naye atapigana na mataifa hayo, kama vile alipopigana zamani siku ya vita. Na hii ndiyo tauni, ambayo BWANA atawapiga watu wote waliofanya vita juu ya Yerusalemu; nyama ya mwili wao itaharibika, wasimamapo juu ya miguu yao, na macho yao yataharibika ndani ya vichwa vyao, na ndimi zao zitaharibika vinywani mwao. —Zekaria 12:2a, 3; 14:3 na 12

Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu? —Warumi 8:31b

## KRISTO NDIYE MTAWALA WA MWISHO ULIMWENGUNI


Kwa maana ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa kutoka mbinguni juu ya uasi wote na uovu wa wanadamu waipingao kweli kwa uovu. —Warumi 1:18

Na upanga mkali hutoka kinywani mwake ili awapige mataifa kwa huo. Naye atawachunga kwa fimbo ya chuma, naye anakanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya Mungu Mwenyezi. Naye ana jina limeandikwa katika vazi lake na paja lake, MFALME WA WAFALME, NA BWANA WA MABWANA. —Ufunuo 19:15, 16

*Mpinga Kristo Atawala Kwa Miaka Michache. Kristo Atawala Hapa Miaka 1,000 Kisha Atatawala Milele.*

Bali watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala pamoja naye hiyo miaka elfu. —Ufunuo 20:6b

Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele. —Danieli 2:44a

*Mataifa Yote Kumuabudu Kristo Bwana!*

Mataifa yote uliowafanya watakuja; watakusujudia Wewe, Bwana, watalitukuza jina lako. —Zaburi 86:9

Kulikuwa na vita mbinguni; Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka, yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake; nao hawakushinda, wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni. Yule joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote; akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye. Nikasikia sauti kuu mbinguni, ikisema, Sasa kumekuwa wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake; kwa maana ametupwa chini mshitaki wa ndugu zetu, yeye awashitakiye mbele za Mungu wetu, mchana na usiku. —Ufunuo 12:7-10

### Silaha Za Ushindi Katika Vita Hivi

Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa. —Ufunuo 12:11

### Maangamizi Ya Shetani Milele

Moto ukashuka kutoka mbinguni, ukawala. Na yule Ibilisi, mwenye kuwadanganya, akatupwa katika ziwa la moto na kiberiti, alimo yule mnyama na yule nabii wa uongo. Nao watateswa mchana na usiku hata milele na milele. —Ufunuo 20:9b na 10



Lusifa angetii katika furaha ya mbinguni milele, lakini alijaribu kutawala Ufalme wa Mungu.
(Soma Isaya 14:13, 14 ukurasa 3.)

### Bwana Kristo Atawala Milele

Ee BWANA, ukuu ni wako, na uweza, na utukufu, na kushinda, na enzi; maana vitu vyote vilivyo mbinguni na duniani ni vyako; ufalme ni wako, Ee BWANA, nawe umetukuzwa, u mkuu juu ya vitu vyote. —1 Mambo Ya Nyakati 29:11

Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa. Lakini kila mmoja mahali pake; limbuko ni Kristo; baadaye walio wake Kristo, atakapokuja. Hapo ndipo mwisho, atakapompa Mungu Baba ufalme wake; atakapobatilisha utawala wote, na mamlaka yote, na nguvu. Maana sharti amiliki yeye, hata awaweke maadui wake wote chini ya miguu yake. Adui wa mwisho atakayebatilishwa ni mauti. —1 Wakorintho 15:22-26

Malaika wa saba akapiga baragumu, pakawa na sauti kuu katika mbingu, zikisema, Ufalme wa dunia umekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atamiliki hata milele na milele. —Ufunuo 11:15



### Shetani huchafua mwili, nafsi kwa ushoga, uuaji wa watoto ambao hawajazaliwa, kupagaa kwa pepo

Wanaume, . . . wakawakiana tamaa, . . . wakapata nafsini mwao malipo ya upotevu wao . . . . —Warumi 1:27

Kuna vitu . . . anavyovichukia BWANA; na mikono imwagayo damu isiyo na hatia. —Mithali 6:16a, 17b

Mara huenda, akachukua pamoja naye pepo wengine saba walio waovu kuliko yeye mwenyewe, nao huingia na kukaa humo; na mtu yule hali yake ya mwisho huwa mbaya kuliko ya kwanza. —Mathayo 12:45a

Mtafute tu Mungu Aliye Hai. Usiite "Mungu mwingine" kujua siku za usoni, Kusoma akili, Kuponywa mwili, au kupata uongozi wa kiroho.

Shetani, muasi Mungu, anahusika na haya yote. Hufanya kazi akitumia watu, maandishi, vitu, na dini za upotevu. Lile analo litoa laweza kuonekana kama kimuujiza na la usaidizi, lakini huleta mtu katika kifungo kikali cha Shetani. Ni Kristo pekee awezaye kukuweka huru.

Kamwe usijitoe kutawaliwa na roho yoyote ambayo si ya Roho Mtakatifu wa Mungu. Amini tu Biblia na Bwana Yesu Kristo. *(Tazama Ufunuo 19:13.)*



### Fundisho lolote linalo elekeza mbali na njia nyembamba ya msamaha, utakaso, na ukombozi kupitia Damu na Utu Wa Kristo ni Ya Uongo Na Udanganyifu

Yesu akajibu, akawaambia, Angalieni, mtu asiwadanganye. Kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu, wakisema, Mimi ni Kristo; nao watadanganya wengi. Na manabii wengi wa uongo watatokea, na kudanganya wengi. —Mathayo 24:4, 5 na 11

Maana wengi huenenda, ambao nimewaambieni mara nyingi habari zao, na sasa nawaambia hata kwa machozi, kuwa ni adui za msalaba wa Kristo; mwisho wao ni uharibifu, mungu wao ni tumbo. —Wafilipi 3:18, 19a

### Samehe Na Usamehewe

Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. —Mathayo 6:14

### Damu Ya Thamani Ya Kristo Hukomboa

Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; . . . bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo. Ambao kwa yeye mmekuwa wenye kumwamini Mungu. —1 Petro 1:18, 19 na 21a



### Kutawaliwa Na Kanuni Ya Dhambi

Kwa maana sisi sote tumekuwa kama mtu aliye mchafu, na matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi. —Isaya 64:6a

### Gadhabu Juu Ya Roho Ya Kutotii

Ambazo mliziendea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, na kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga, roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi; ambao zamani, sisi sote nasi tulienenda kati yao, katika tamaa za miili yetu, tulipoyatimiza mapenzi ya mwili na ya nia, tukawa kwa tabia yetu watoto wa hasira kama na hao wengine. —Waefeso 2:2, 3

### Shetani Hutawala Juu Ya Wasiookoka

Lakini ikiwa injili yetu imesitirika, imesitirika kwa hao wanaopotea; ambao ndani yao mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini, isiwazukie nuru ya injili ya utukufu wake Kristo aliye sura yake Mungu. —2 Wakorintho 4:3, 4

### Katika Kristo Ndio Ushindi

Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu. —Warumi 8:1



Lile konde ni ulimwengu; zile mbegu njema ni wana wa ufalme; na yale magugu ni wana wa yule mwovu. —Mathayo 13:38

Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi, na tamaa za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda. —Yohana 8:44a

### Katika Adamu, Tunamuasi Mungu

Mtu asiye pamoja nami yu kinyume changu; na mtu asiyekusanya pamoja nami hutapanya. —Mathayo 12:30

### Hii Ndio Sababu Ni Lazima Tuzaliwe Upya Katika Roho Wa Kristo

Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazama! yamekuwa mapya. —2 Wakorintho 5:17

Kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua, nao wanifuata. Nami nawapa uzima wa milele. —Yohana 10:27, 28a

### Jitoe Kwake Bwana Yesu Sasa

Tazama, wakati uliokubalika ndio sasa; tazama, siku ya wokovu ndiyo sasa. —2 Wakorintho 6:2b

Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote. —1 Yohana 1:9

Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je! ni dhiki, au shida, au adha, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga? Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda. —Warumi 8:35 na 37

Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu. —1 Yohana 5:4

### Huwapa Thawabu Wanaoshinda

Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa. Yeye ashindaye nitampa baadhi ya ile mana iliyofichwa, nami nitampa jiwe jeupe, na juu ya jiwe hilo limeandikwa jina jipya asilolijua mtu ila yeye anayelipokea. —Ufunuo 2:17

Na yeye ashindaye, na kuyatunza matendo yangu hata mwisho, nitampa mamlaka juu ya mataifa. —Ufunuo 2:26

### Wewe Ni Wa Muhimu Sana Kwa Mungu. Kalvari Inathibitisha Hivyo! Mungu Ni Wa Muhimu Sana Kwako!

Si kwamba twatosha sisi wenyewe kufikiri neno lo lote kwamba ni letu wenyewe, bali utoshelevu wetu watoka kwa Mungu. —2 Wakorintho 3:5



### Tokea Na Kristo Katika Utukufu

Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu, Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi. Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu. Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu. Basi, vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi, uasherati, uchafu, tamaa mbaya, mawazo mabaya, na kutamani, ndiyo ibada ya sanamu: kwa ajili ya mambo hayo huja ghadhabu ya Mungu. —Wakolosai 3:1-3 na 4-6

### Au Ulaaniwe Pamoja Na Shetani Milele

Kisha atawaambia na wale walioko mkono wake wa kushoto, Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake. —Mathayo 25:41

Wadhalimu watarejea kuzimu, naam, mataifa yote wanaomsahau Mungu. —Zaburi 9:17

Na mkono wako ukikukosesha, ukate; ni afadhali kuingia katika uzima u kigutu, kuliko kuwa na mikono miwili, na kwenda zako jehanum, kwenye moto usiozimika. —Marko 9:43



### Jinyenyekeze

Saa ile wanafunzi wakamwendea Yesu wakisema, Ni nani basi aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni? Akaita mtoto mmoja, akamweka katikati yao, akasema, Amin, nawaambia, Msipoongoka na kuwa kama vitoto, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni. Basi, ye yote ajinyenyekeshaye mwenyewe kama mtoto huyu, huyo ndiye aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni. —Mathayo 18:1-4

### Tubu Dhambi

Yohana alitokea, akibatiza nyikani, na kuuhubiri ubatizo wa toba liletalo ondoleo la dhambi. Hata baada ya Yohana kutiwa gerezani, Yesu akaenda Galilaya, akihubiri Habari Njema ya Mungu, akisema, Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini Injili. —Marko 1:4 na 14, 15

Nawaambia, Sivyo; lakini msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo. —Luka 13:3

Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana. —Matendo 3:19

Tokea wakati huo Yesu alianza kuhubiri, na kusema, Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia. —Mathayo 4:17

*(Inaendelea ukurasa wa pili.)*

## MPOKEE KRISTO KAMA MWOKOZI WAKO LEO

### Jitoe Kwake Yesu Kristo

Umkabidhi BWANA njia yako, pia umtumaini, naye atafanya. —Zaburi 37:5

Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. —Yohana 3:16

Wakamwambia, Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako. —Matendo 16:31

### Mumgu Huwapa Nguvu Kuwa Wanawe

Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake. Amani nawaachieni; amani yangu nawapa. —Yohana 1:12 na 14:27a

### Mkiri Kristo Waziwazi

Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu. Kwa maana andiko lanena, Kila amwaminiye hatatahayarika. —Warumi 10:9-11

Scripture text reprinted from the Bible in Kiswahili by permission of United Bible Societies Africa Regional Centre, Nairobi, Kenya.

Published in numerous languages by World Missionary Press as God supplies funds in answer to prayer. If you would like more copies for careful distribution, please write to us in English.

**World Missionary Press, Inc.**
**P.O. Box 120**
**New Paris, IN 46553-0120 USA**

www.wmpress.org

Kiswahili SVC